

# END OF TERM 1 EXAMS

## KISWAHILI

### FORM TWO

TIME: 1 ½ HOURS

NAME.....ADM NO:.....

SIGN..... INDEX NO:.....

#### MAAGIZO

Jibu maswali yote.

1. UFAHAMU

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Changamoto kubwa inayowakabili watu wengi katika mataifa yanayoendelea ni suala la chakula. Suala hili linaweza kuangaliwa katika sawia mbili tofauti. Kuna tatizo linalofungamana na uhaba wa chakula chenyewe. Uhaba huu unaweza kutokana na utegemezi mkubwa kwa zaraa kama nyenzo kuu ya uzalishaji wa chakula.

Zaraa katika mataifa mengi hususan yanayoendelea, hutegemea mvua. Kupatikana kwa mvua huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ulimwnguni. Matendo na amali za watu kama ukataji wa miti na uchafuzi wa mazingira huwa na athari hasi kwenye tabianchi hiyo. Mabadiliko ya tabianchi huweza kuvyaza ukama kutokana na **ngambi ya mvua**.

Kibinimethali kutokea wakati mafuriko yanapotokea na labda kuyasomba mazao mashambani na kusababisha baa la njaa. Hali hizi mbili husababisha matatizo makubwa ya chakula na kuathiri pakubwa suala zima la usalama wa chakula. Ili kuzuia uwezokano wa kuwepo kwa shida hii, pana haja ya kuwepo kwa mikakati na sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Kwa mfano, pana haja ya kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka **adha** inayosababishwa na ukosefu wa mvua. Kwa upande

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657**

mwingine, sharti zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

Changamoto nyininge inahusiana na usalama wa chakula chenyewe. Chakula kilichosibikwa na vijasumu au kwa njia nyininge ile huweza kumdhuru anayehusika. Msibiko wa chakula unatokana na vyanzo tofauti. Mathalan uandalizi wa chakula kilichochoafuliwa na choo, kutozingatia mbeko za usafi, uandaaji wa chakula na kukiweka katika hali ya uvuguvugu kabla ya kukipakua – hali inayochochea ukuaji wa viini na ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema.

Ili kuepuka uwezekano wa kuathirika, pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula na uandalizi unaofaa. Fauka ya hayo, vyombo cya uandalizi view safi, kanuni za usafi zifuatwe, upikaji na uandaaji uwe kamilifu. Hali hii isipozingatiwa, siha za raia wenyewe zitaathirika pakubwa.

**Maswali.**

1. Taja aina mbili za kuangalia suala la chakula katika mataifa yanayoendelea. (alama 2)
  
2. Taja hatua mbili zinazoweza kuchukuliwa kupambana na tatizo la chakula. (alama 2)
  
3. Eleza jinsi nne tofauti namna chakula kinavyoweza kuwa si salama? (alama 4)
  
4. Kwa nini ni rahisi kukipakua chakula baada ya kukiandaa tu? (alama 1)
  
5. Ni mapendekezo gani anayoyatoa mwandishi kuhakikisha kuwa chakula kinafaa? (alama 4)

## **MATUMIZI YA LUGHA**

1. Kwa kutoa mifano eleza tofauti kati ya: (alama 2)
  - i. Silabi fungo
  - ii. Silabi wazi
2. Onyesha sauti zenyе sifa zifuatazo: (alama 2)
  - i. Kipasuo cha ufizi
  - ii. Kikwamizo cha kaakaa laini
3. Tambua aina ya nomino katika sentensi zifuatazo. (alama 2)
  - i. Mchanga hufanya miti kumea.
4. Bainisha mofimu katika kitenzi. (alama 2)  
Kilipikika
5. Tambua vivumishi katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani. (alama 2)
  - i. Mtoto wake ameng'oka jino.
  - ii. Msemo wenge tafsida hupendwa.
6. Andika kinyume cha: (alama 1)  
Tulinunua nguo aliizozianika jana.
7. Nomino 'uki' iko kwenye ngeli gani. (alama 1)

8. Ainisha vitenzi kwenye fungo zifuatazo: (alama 3)  
i. Yatakuwa yangali yanakoma.
- ii. Maria na Atieno ni wanafunzi watiifu.
9. Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)  
i. Rais ametutembelea mara sita mwaka huu.
- ii. Nendeni haraka shuleni.
10. Eleza maana inayojitokeza kwenye sentensi ifuatayo. (alama 1)  
i. Waiteni watu wale.
11. Tumia kiwakilishi kisisitizi kutungia sentensi ya wingi wakati uliopita. (alama 2)

### **ISIMU JAMII**

#### **Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Haya ng'ara ... Ng'ara leo! Nguo motomoto. Ng'ara leo kwa bei rahisi. Hamsini hamsini shati. Kuona ni bure. Bure kwa bure. Shika mwenyewe ujionee. Bei nafuu. Bei ya starehe. Haya, haya. Usikose mwanangu! Hamsa! Hamsa! Fifty!Hamsa! Fifty! Hamsa na nyingine.

#### **Maswali.**

- a. Bainisha sajili ya mazungumzo haya. (alama 1)
- b. Eleza sifa nane za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 4)

**FASIHI SIMULIZI.**

- a. Fafanua maigizo. (alama 2)
- b. Ainisha kipera cha maigizo. (alama 4)
- c. Eleza sifa za maigizo. (alama 4)